Toleo 91 - Muharram 1446 H / Agosti 2024 M

# Jarida la UQAB

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Uchaguzi nchini Marekani na Uingereza Unashindana katika Kulenga Uislamu na Waislamu

**HABARI NA MAONI**
Mwito wa Mabadiliko: Uislamu Mfumo pekee Usiocheza Shere na Kuhujumu Maisha ya Watu

**MATOLEO**
Wakenya Amkeni

**MATOLEO**
Marekani Inatafuta Ushindi Madhubuti nchini Afghanistan



uqab.info
uqab_htk
UQABMagazine

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

Afisi ya Habari Kenya

حزب التحرير

Hizb ut Tahrir

KUMB: 046/1445 Jumamosi, 30 Dhu al-Hijjah 1445 H 06/07/2024 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Uchaguzi nchini Marekani na Uingereza Unashindana katika Kulenga Uislamu na Waislamu

Katikati ya uungaji mkono wa Marekani na Uingereza kwa mauaji yanayofanywa na umbile la Kiyahudi, ambalo liliasisiwa na Himaya ya Uingereza yenyewe, na baada ya zaidi ya miezi tisa ya uungaji mkono wao kwa umwagaji damu wa Waislamu mjini Gaza, kampeni za uchaguzi wa rais na chama zinaendelea hivi sasa nchini Marekani na Uingereza. Katika kampeni hizi, wale wanaojiona wanastahili zaidi kuongoza dola hizi mbili za kikoloni, ambazo zimesababisha njaa na udhalilifu kwa mataifa, zikifanya juhudi zao kubwa kupata tonge ya chakula, tama la maji, na muangaza ambao sasa unazima zaidi kuliko kumulika katika miji mikuu na miji mikuu ya nchi za Kiislamu, kama vile Cairo na Karachi.

Leo, nchini Marekani, wanasiasa wenye mikono inayochuruzika damu ya Waislamu wanashindana, bila haya kutangaza uungaji mkono wao kwa dola ya kihalifu, umbile la Kiyahudi, na hata kushindana katika kutuma msaada zaidi kwa umbile hili. Wanalaumiana wao kwa wao kwa mapungufu ya kuwapa mabomu na silaha zinazoua watoto na wanawake wasio na hatia katika Ardhi Iliyobarikiwa ya Palestina. Licha ya Biden kuendeleza aina zote za uungaji mkono wa kijeshi, kifedha, kisiasa na vyombo vya habari kwa umbile la Kiyahudi, mpinzani wake Trump alimdhihaki, akimwita “Mpalestina” akimaanisha kushindwa kwake kuunga mkono mauaji ya halaiki huko Gaza! Alidokeza kwamba ataongeza uungaji mkono kwa umbile la Kiyahudi ili kufikia ndoto yake ya ubwana juu ya Umma wa Kiislamu katika ardhi iliyobarikiwa ya Palestina na kuiangamiza.

Ama Uingereza, pande zote mbili (Conservatives and Labour) zinashindana kwa kutumia suala la wahamiaji ambao wengi wao wanatoka katika nchi za Kiislamu wanaoteswa na serikali zao ambazo ni Vibaraka wa Uingereza na Marekani. Wanaahidi kuwafukuza wakimbizi na wanyonge au kupunguza utitiri wao, na kuwaacha wakabiliane na hatima yao katika bahari. Mkruseda wa Kibaniani Sunak, Waziri Mkuu wa Uingereza, alikwenda kwa umbile la Kiyahudi kwa ndege ya kijeshi iliyobeba vifaru na silaha, akijisifu juu ya kuongoza vita vya kikruseda vya Ulaya ili kuivamia ardhi iliyobarikiwa kwa mara nyingine tena!

Hizi ni kampeni za uchaguzi katika dola kubwa za Kikruseda, kampeni zinazotoa wito wa kuuawa kwa Waislamu na kuungwa mkono kwa wauaji wao, na kuteswa wanyonge na wakimbizi miongoni mwao. Je, kuna manufaa yoyote kwa Waislamu katika chaguzi hizi? Je, wanaweza kupata haki kati ya hawa walaghai? Ni dhahiri shahiri kwamba Waislamu hawana hisa katika chaguzi hizi; wao ni wahanga na kafara. Tofauti kati ya Conservatives na Labour na kati ya Republicans na Democrats iko kwenye utaratibu na chombo cha kuchinja, hivyo ni jambo lisilowezekana kuwa mtu anayetaka kutuua kwa mizinga na vifaru ni bora kuliko anayetaka kutuua kwa njaa, kuzama majini, au njia nyenginezo!

Kumchagua yeyote kati ya washindani hawa hairuhusiwi kabisa, bila kujali tafsiri za wanazuoni wa sultan na waabudu pauni na dolari. Hakuna ikhtilafu kwamba kumchagua yeyote kati yao ni leseni kwao kuwaua Waislamu zaidi na kuongeza mateso yao duniani kote, hasa katika ardhi iliyobarikiwa ya Palestina. Yeyote anayetaka kuwa mshirika wa wahalifu hawa ateue mtu wa kumpigia kura. Kwa kufanya hivyo atajidhulumu nafsi yake na hatakuwa na nafasi ya kuwa kipenzi cha Mwenyezi Mungu.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْيَهُودَ وَالنَّصَارَىٰ أَوْلِيَاءَ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ مِنْكُمْ فَإِنَّهُ مِنْهُمْ إِنَّ اللهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ

**“Enyi mlio amini! Msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa ni marafiki. Wao ni marafiki wao kwa wao. Na miongoni mwenu mwenye kufanya urafiki nao, basi huyo ni katika wao. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wenye kudhulumu.”** [Surat Al-Ma’ida:51]

***Endelea... UK 3***

Waislamu wanaoishi katika nchi za Magharibi, zikiwemo Marekani na Uingereza, wana wajibu wa kutetea matukufu ya Waislamu kutokana na ukiukaji wa wahalifu hao. Hili haliwezi kufikiwa kwa kujihusisha na njama zinazosukwa na wagombea hao kwa kumpigia kura yeyote kati yao, kwani wote ni sura za sarafu moja ya riba. Badala yake, inapaswa kufanywa kwa kuwashutumu kupitia njia na mbinu zote halali, kama inavyoruhusiwa na sheria za nchi hizo zenyewe. Dori hii, pamoja na kuwa ni wajibu kwa taifa lao na watu wanaodhulumiwa duniani, wakiwemo watu wa ardhi iliyobarikiwa na Gaza, pia ni kitendo adhimu kisichopingwa na watu wowote wenye nia ya haki na wale wenye maadili miongoni mwa wanafikra huru katika nchi za Magharibi.

Siku hizi sauti zao zimekuwa kubwa kutokana na kufichuliwa kwa wanasiasa na vyama vyao vya kisiasa na kufichuliwa kwa kauli mbiu potofu walizokuwa wakitoa kwa muda mrefu kama vile uhuru, haki za binadamu na demokrasia. Hata hivyo, wako katika haja kubwa ya Waislamu wanaoishi miongoni mwao ili kuwaongoza kwenye njia iliyo sawa na kuuwasilisha kwao Uislamu kama hadhara badali ya kuchukua nafasi ya mfumo wa kibepari ambao umesababisha wanadamu na watu wa Magharibi kuteseka.

Hii ndio dori ya Waislamu katika nchi za Magharibi: dori ya wabebaji wa ujumbe wa haki kwa watu wote, ambao kwao wanafanya wema kwa watu wenye nia ya haki katika nchi hizo. Kuwepo kwao Magharibi kwa hivyo kunakuwa chanya kwa viwango bora vinavyomridhisha Mwenyezi Mungu, na kunawatoa watu wa nchi hizo kutoka kwenye giza la ubepari na dhulma zake hadi kwenye nuru ya Uislamu na uadilifu wake. Kwa njia hii wanatekeleza wajibu wao wa kufikisha ujumbe badala ya kujihusisha na mchezo mchafu wa kisiasa wa Kimagharibi ambao msingi wake ni mafuvu ya Waislamu na kuwanyima watu haki zao. Hao ni walinganizi kwa Mwenyezi Mungu ili kuwaokoa watu, na sio kuyumba katika jamii zilizo potea na kupotoka. Mwenyezi Mungu Mtukufu asema:

وَلْتَكُنْ مِنْكُمْ أُمَّةٌ يَدْعُونَ إِلَى الْخَيْرِ وَيَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ

**“Na uwe kutokana na nyinyi umma unao lingania kheri na unao amrisha mema na unakataza maovu. Na hao ndio walio fanikiwa.”** [Surat Aal-i-Imran:104].

**Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:

# Kampeni “Enyi Umma; Kilio Wanacholia Wafungwa wa Dhamiri nchini Uzbekistan!”

Vyombo vya usalama nchini Uzbekistan vimewakamata tena wanachama 23 wa Hizb ut Tahrir na kuendelea na taratibu za kesi zao Mei 9 mwaka huu kwa mashtaka yale yale waliyoshtakiwa wakati wa enzi ya dhalimu aliyefariki Karimov, ambayo kwayo walitumia karibu miaka 20 jela na mateso tangu 1999 - 2000 M. Licha ya madai yote yaliyotolewa na Mirziyev miaka iliyopita, ambapo alidai kuwa anapinga mateso na unyanyasaji dhidi ya wafungwa, na kwamba yuko kwenye njia ya kuunganisha uhuru wa fikra na itikadi na kupambana na ukamataji kiholela, tabia ya hivi karibuni ya serikali ya Uzbekistan chini ya uongozi wake inaonyesha kwamba inafuata nyayo za Karimov aliyekufa katika kuwa na uadui na Uislamu na wale wote wanaoulingania, na kuwatesa mashababu wa Hizb ut Tahrir kwa kutumia mbinu za kidhalimu na za kikatili ambazo mtangulizi wake wa uhalifu Karimov ilizitumika hapo awali.

Mashababu walikamatwa kiholela na kwa njia za kinyama na za kikatili kwa haki zao na kuwalazimisha kuungama tuhuma walizobambikiziwa, ambapo waliwaweka mifuko kwenye vichwa vyao na kuweka shinikizo kali juu yao, na walilazimishwa kutia saini maungamo hayo yaliyotayarishwa mapema chini ya tishio la kuletwa mke wa mmoja wao afisini na kumbaka. Na tishio jengine lilikuwa kumleta mtoto wa shababu mwengine anayesoma nje ya nchi, hadi Uzbekistan kupitia ubalozi, na kumleta mtoto wa shababu mwengine katika Afisi ya Mambo ya Ndani ili kumlazimisha kusaini hati ya kukiri, na kumtesa shababu mwengine kwa shoti ya umeme.  Pia mashababu wapya 16  walikamatwa katika majimbo ya Tashkent, Andijan, Hawqan, Karshi na Samarkand, na kufikishwa Tashkent na kuchunguzwa, kwa tuhuma zinazohusiana na kufanya vurugu na ugaidi!

Tuhuma za ugaidi na kutekeleza unyanyasaji dhidi ya mashahabu wa Hizb ut Tahrir ni wazi kuwa ni uzushi na uongo. Hizb ut Tahrir na mashababu wake hawafanyi fujo wala ugaidi, na wala hizb haijawahi kufanya hivyo tangu kuasisiwa kwake mwaka 1953 M. Haifanyi hivi sio kwa sababu ya kuogopa kwake tawala hizi au kujaribu kuridhiana na tawala dhalimu, bali kwa sababu inamwabudu Mwenyezi Mungu kwa njia yake ili kuregesha maisha kamili ya Kiislamu, ambayo ni njia ya kifikra na kisiasa ambayo iliifuatwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw). Kwa hiyo, tawala zote za ukandamizaji na za kipolisi katika nchi za Kiislamu na hata katika nchi za Magharibi hazikuweza kuthibitisha shtaka la ugaidi au vurugu dhidi ya Hizb ut Tahrir na mashababu wake, licha ya majaribio yao ya mara kwa mara. Lakini ni chuki inayofurika kutoka katika nyoyo za watawala wahalifu, ambayo inawasukuma kudanganya macho na masikio yao kutokana na kutaka kulipiza kisasi dhidi wabebaji wa mradi unaokuja wa Kiislamu, mradi wa Khilafah Rashida ya pili kwa njia ya Utume. Watawala wa Waislamu, chini ya uongozi wa mabwana zao, viongozi wa uhalifu na ukoloni nchini Marekani, Uingereza, Urusi, Ufaransa na Ujerumani, wanaupiga vita mradi wa Uislamu na kuzikanyaga sheria na kanuni zao wanazozipigia debe na kuzinadi kwa ulimwengu (uhuru, demokrasia, haki za binadamu) linapokuja suala la ubebaji dawah miongoni mwa mashababu wa Hizb ut Tahrir.

Kuregea kwa Mirziyev katika mkabala wa ukandamizaji, ukamataji, na utesaji katika nyayo za Karimov aliyekufa kunaonyesha kwamba jambo hilo ni utekelezaji wa matamanio na sera za viongozi wa kikoloni nchini Urusi na Marekani, na kwamba watawala wetu, kama kawaida yao, hawamiliki maamuzi yao na si chochote ila wafuasi wa vibaraka wa ukoloni.

Sisi katika Hizb ut Tahrir tunauonya utawala wa Mirziyev dhidi ya kuregea kwenye sera ya ukandamizaji na ukatili ambayo utawala wa Karimov uliitumia dhidi ya Uislamu na wabebaji dawah yake. Hii ndiyo njia ya wahalifu na haitawanufaisha, bali itazidisha hasira za Umma juu yake na kujaalia kuangamia kwake, Umma wa Kiislamu sasa unatazamia siku hiyo utakapokombolewa kutokana na ukoloni na kuregea katika sheria ya Mola wake Mlezi, kama katiba, sheria na maisha, na Umma leo uko karibu zaidi kuliko wakati mwingine wowote kufikia lengo na matumaini yake. Hivyo basi, Mirziyev lazima awaachilie huru mashababu wetu mara moja na bila kuchelewa, aache kuwatesa wale wanaobeba ujumbe na kuwa na uadui kwa mradi wa Uislamu, na ajifunze kutoka kwa wale waliokuja kabla yake, hakika mwisho mwema ni kwa wachaMungu hata kama mila yote ya ukafiri itakusanyika pamoja, na Mwenyezi Mungu atainusuru dini yake, hata kama ni baada ya muda kidogo, Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema

كَتَبَ اللَّهُ لَأَغْلِبَنَّ أَنَا وَرُسُلِي إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ

**“Mwenyezi Mungu ameandika: Hapana shaka Mimi na Mtume wangu tutashinda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye kushinda.”** [Mujadala: 21]

**Ijumaa, 29 Dhu al-Hijjah 1445 H sawia na 5 Julai 2024 M**

# Wakenya Amkeni



Kenya, shamba la kikoloni, kwa mara nyingine imo katika mchafuko na mtikisiko kwa kuwa mchezo wa bahati nasibu wa kidemokrasia umezunguka nyuzi 360! Walioko madarakani na walioko barabarani wakiandamana wanalaumiana, huku madai yakielekezwa kwa Mswada wa Kifedha wa 2024 ulioandaliwa kwa maelekezo ya Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) (Business Daily, 28 Juni 2024)! Mswada huo unapendekeza mikakati ya kuzidisha ukusanyaji wa ushuru ambao unatajwa kuwa ni wenye kukandamiza na kuwadidimiza raia katika umasikini zaidi! Licha ya Rais wa Kenya, Ruto kuandikia bunge ili kuuondosha , bado raia hawaja punguza hasira na kusitisha maandamano.

Ukweli ni kwamba Mswada huo ulikuwa tu ni sanduku la Pandora. Umefichua kufeli kupindukia kwa nidhamu ya kiuchumi ya kirasilimali ya kisekula ya Kimagharibi sio tu nchini Kenya na Afrika kwa ujumla hata katika miji ya Kimagharibi kwa kuwa msingi wake ni kupatiliza na kupora rasilimali za wenyeji na kuwakandamiza watu kwa maagizo ya warasilimali wakubwa. Kila kitu na kila mtu ni mtumwa kwa maslahi ya mabwana wakoloni Wamagharibi. Hivyo basi, marais au watawala wote wapo kama wasimamizi wa shamba la kikoloni, mabaraza yao ni wasaidizi wao! Raia waliobakia ni wafanyakazi ndani ya mashamba! Haishangazi, hapa nchini Kenya tangu 'uhuru bandia wa bendera' mnamo 1963, bado tunazirudia sera na sheria zilizoandikwa na Wamagharibi ili kusimamia shamba!

Suala na suluhisho msingi sio KUJIUZULU kwa serikali ya Kenya na kubadilisha nyingine. Chochote kinachofanana na hilo itakuwa ni mabadiliko ya kiviraka yaliyo na matokeo kama yanayo shuhudiwa hivi sasa. Njia mbadala ya kimsingi ni kubadilisha kikamilifu mfumo wa kirasilimali wa kisekula wa Kimagharibi na nidhamu zake ambazo utekelezaji wake unaleta majanga duniani kote hivi sasa. Unatakiwa kubadilishwa kwa mfumo unaochipuza kutoka kwa Muumba wa ulimwengu, mwanadamu na uhai ikimaanisha Allah (swt) sio Yesu, mtume wa Allah (swt).

Wacha nitoe mlinganisho; sote tunakubaliana kwamba pikipiki ili kuwaka tunahitaji petroli. Hata hivyo, tukisonga mbele na kutia ima maji au dizeli na kutarajia pikipiki kuwaka, itakwama kabisa na utadhaniwa kuwa mwendawazimu. Je, sisi sio wendawazimu kushiriki katika mchezo wa kidemokrasia ilhali Muumba wa ulimwengu, mwanadamu na uhai ana maamrisho ya wazi kuhusu namna gani tuweze kuendesha maisha yetu katika uhai huu mfupi?! Chaguo pekee la uhakika ni kukata mizizi ya mfumo wa kirasilimali wa kisekula na nidhamu zake na badala yake tujiunge na ulinganizi wa utekelezaji wa nidhamu ya Kiislamu kama inavyolinganiwa na chama cha kisiasa cha Kiislamu cha Kiulimwengu cha Hizb ut Tahrir. Mfumo wa Kiislamu na nidhamu zake zinapeana utulivu kwa watu wote pasina kuzingatia dini zao na viwango vya kiuchumi. Ni suluhisho pekee na mengine sio chochote bali ni natija ya akili yenye kikomo ya mwanadamu kwa mfano urasilimali, ukomunisti na ujamaa.

Lazima tuseme imetosha kushiriki mchezo wa bahati nasibu na unaoendeleza shida, mauaji, ukandamizaji na ukatishaji tamaa wanadamu na kupora rasilimali zao kupitia majambazi wachache! Tuamkeni na tuchukue hatua kwa kuachana na wakoloni Wamagharibi na mfumo wao na nidhamu zake!


**Written for the Central Media Office of Hizb ut Tahrir**
**by**

**Ali Nassoro (Abu Taqiuddin)**
**Member of the Central Media Office of Hizb ut Tahrir**

# HABARI NA MAONI
# Mwito wa Mabadiliko: Uislamu Mfumo pekee Usiocheza Shere na Kuhujumu Maisha ya Watu



**Habari:**

Kenya, imekumbwa na maandamano makubwa katika masiku ya hivi majuzi baada ya bunge kupitisha mswada wa kuongeza ushuru – ikiwa ni pamoja na mahitaji ya kila siku kama vile mafuta ya kupikia, nepi, na mkate – kwa idadi ya watu ambao tayari wanakabiliwa na mfumko wa bei na viwango vya juu vya ukosefu wa ajira. Rais Ruto alikataa kutia saini mswada huo baada ya maandamano makubwa ambayo kufikia sasa watu 39 wameuawa na makumi ya wengine kujeruhiwa.

**Maoni:**

Maandamano ya (Gen Z) yalichochewa na kuwasilishwa kwa mswada mpya wa fedha ambao ungetoza ushuru wa kuadhibu kwa mahitaji ya kila siku, ikiwa ni pamoja na sukari, mkate na mafuta ya kupikia – sera ambayo ingeendeleza athari kubwa ya kiuchumi kwa wakenya wengi masikini. Mswada huo huo ulitenga kando kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya ukarabati wa makaazi ya rais na matumizi mengine makubwa.

Mapema mwezi Juni, Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) ulifikia makubaliano ya awali juu ya utoaji wa mikopo ambayo uliitaka serikali ya Kenya kuongeza mapato yake; Kenya ikawa na lengo la kupata dolari bilioni 2.7 za ziada. Kwa hivyo Nairobi haikuwa na njia nyengine ila tu kupeleka maumivu kwa raia wake kupitia sera za ushuru kandamizi ambazo zingeendeleza kuathiri zaidi maskini. Wala si Kenya pekee: Zaidi ya watu bilioni 3 kote ulimwenguni wanaishi katika nchi ambazo zinatumia zaidi mapato yake kulipa madeni yao kuliko matumizi ya umma katika sekta ya elimu au afya.

Ingawa kichocheo cha maandamano haya ni sera mbovu za kifedha na tabaka la kisiasa lenye uchu, vyombo vya habari vinaendelea kuonesha kwamba waandamanaji wanawakilisha hisia za vijana wa Kenya, lakini vinashindwa kuona mfumo mbovu wa kiuchumi wa Ubepari. Kwa upande wa vijana, ambao wanaonekana matarajio yao yako gizani, na kukatishwa tamaa na tabaka la kisiasa lenye ulafi lisilojali maslahi yao—vijana wanaonekana dhahiri kutokuwa na viongozi bali wafanyibiashara, na wamejipanga wenyewe mtandaoni, wakifanya mikutano mikubwa ya mtandaoni, na wameingia mitaani bila uoga. Maandamano ambayo hayajawahi kushuhudiwa nchini Kenya, ni dalili wazi ya kushindwa kabisa kwa wanasiasa wa Kidemokrasia pamoja na mfumo wao wa kibepari – mfumo wa kiuchumi ambao unasukuma ukatili wa wanasiasa na ulafi, hivyo basi kuwanyima raia wa kawaida kukidhi mahitaji ya kimsingi.

Ukoloni wa Magharibi uliunda dhana inayofunga mipaka ya mabadiliko kwenye chaguzi, mageuzi ya katiba na hatua za kiuchumi, kwa maana hii waandamanaji wataingia katika mtego huo huo wa Magharibi yaani kuiga Magharibi wanaojiona kuwa wao ndio wanaomiliki hatima ya 'mabadiliko' yoyote.

Mabadiliko ya kweli ambayo vijana sio tu nchini Kenya bali ulimwengu mzima wanapaswa kuyataka ni mfumo ulio na suluhisho la wazi la matatizo yanayowakabili wanadamu. Mfumo huu ni Uislamu ambao haukuacha maisha ya watu kuchezewa na kutumiwa kirahisi na tabaka la wanasiasa walafi wanaohubiri Demokrasia kama njia ya kuhadaa watu kwa lengo la kutimiza ubinafsi wao. Mwenyezi Mungu (swt) alimtuma Mtume wake wa mwisho (saw) akilingania watu maisha ya kweli ya Kiislamu wala sio maisha ya hadaa yaliyosheheni uwajibikaji wa kirongo na kushiriki katika siasa za domokaya.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Kenya**

# Marekani Inatafuta Ushindi Madhubuti nchini Afghanistan



Serikali ya Marekani, kupitia taasisi za kimataifa, hasa Umoja wa Mataifa, inalenga kupata ushindi madhubuti. Ni ushindi ambao haikuweza kuupata, licha ya zaidi ya miaka ishirini ya vita dhidi ya Uislamu na Mujahidina nchini Afghanistan. Utafutaji ushindi huu ulianza pale Marekani ilipoiruhusu Qatar kuwa mwenyeji wa vuguvugu la Taliban, na kufungua afisi kwa ajili ya vuguvugu hilo huko Doha mwaka 2013. Kupitia afisi hii, Marekani ilijihusisha kisiasa na harakati hiyo, na kusababisha duru kadhaa za mazungumzo yaliyohusisha Marekani na waamuzi, ukiwemo ujasusi wa Pakistan. Hatimaye, pande zote mbili zilikubali kukabidhi nchi kwa vuguvugu la Taliban, pamoja na kujiondoa kwa vikosi vya kijeshi vya Magharibi, lakini kwa mwendelezo wa "kipote cha washawishi wa wakuu serikalini" (Deep State) waaminifu kwa Marekani. Kipote hicho cha washawishi kilianzishwa kibaraka wa Marekani na Afghanistan ambaye Marekani ilimlimpandisha madarakani, Hamid Karzai, pamoja na waziri wake wa mambo ya nje Abdullah, Abdullah, ambaye alisimamia Baraza Kuu la Maridhiano ya Kitaifa la Afghanistan, pamoja na rais wa zamani Rabbani.

Ili kuhakikisha kwamba Marekani na dola za kikoloni za Magharibi zinahakikishiwa tena kuhusu mustakabali na uhalisia wa dola ya "kitaifa" ya Afghanistan, baada ya Mkataba wa Doha, walilazimisha masharti, mipango na miundo ya serikali, juu ya utawala wa harakati ya Taliban. Hii ilikuwa ni kuhakikisha kwamba dola ya harakati hiyo haitakuwa tofauti na dola nyengine za sasa katika Ulimwengu wa Kiislamu, ambazo zote zinatii Magharibi. Lengo muhimu zaidi lilikuwa ni kuzuia vuguvugu la Taliban kuunda serikali ya Kiislamu, au kutangaza dola ya Kiislamu inayotawala kipekee na kikamilifu kwa Quran Tukufu na Sunnah ya Mtume, njia ambayo maelfu ya Mujahidina wa Afghanistan waliuawa kishahidi kwa ajili yake.

Licha ya vuguvugu la Taliban kukubaliana na Makubaliano ya mwisho ya Doha kabla ya kuchukua madaraka mwaka 2021, na kukubali kuanzisha dola ya "kitaifa" ya Afghanistan, yenye sura ya Kiislamu, badala ya dola ya Kiislamu, Marekani haikukubali harakati na serikali yake kuingia katika klabu ya wakoloni wa Magharibi, kama wasaidizi wake wengine katika nchi

*Endelea... UK 8*

mbalimbali za Kiislamu. Badala yake, Marekani iliendelea kuongeza masharti na maagizo kwa serikali hiyo. Katika kujibu, serikali ya harakati ya Taliban iliendelea kukubali na kutekeleza maagizo haya kama yalivyo. Kukubali na kutekeleza huku ni kwa kiwango ambacho Taliban hawakujiepusha tu kutabikisha hukmu za Shariah, bali pia walijiunga na muungano wa Magharibi katika vita vyake vya msalaba dhidi ya Uislamu. Serikali hiyo ilimuandama, kumfunga, na kumtesa yeyote anayetaka kutekelezwa kwa hukmu za Shariah, kinyume na madai yake ya hapo awali. Ilitaka hata wale wanaofanya kazi ya kusimamisha Khilafah kwa Njia ya Utume "watubu" na waache juhudi tukufu za kuhukumu kwa yale yote aliyoteremsha Mwenyezi Mungu (swt), kazi ya Mitume na Mitume madhubuti (as)! Kwa hivyo, harakati ya Taliban ilitumbukia katika mtego wa Magharibi, kama ilivyotajwa katika aya hii,

[وَلَنْ تَرْضَى عَنْكَ الْيَهُودُ وَلَا النَّصَارَى حَتَّى تَتَّبِعَ مِلَّتَهُمْ قُلْ إِنَّ هُدَى اللَّهِ هُوَ الْهُدَى وَلَئِنِ اتَّبَعْتَ أَهْوَاءَهُمْ بَعْدَ الَّذِي جَاءَكَ مِنَ الْعِلْمِ مَا لَكَ مِنَ اللَّهِ مِنْ وَلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ]

**"Mayahudi hawawi radhi nawe, wala Wakristo, mpaka ufuate mila yao. Sema: Hakika uwongofu wa Mwenyezi Mungu ndio uwongofu. Na kama ukifuata matamanio yao baada ya ujuzi ulio kwisha kujia, hutapata mlinzi wala msaidizi kwa Mwenyezi Mungu."** [Surah al-Baqarah 2:120]. Kufuata njia ya maisha ya Mayahudi na Manaswara haikufungika tu katika imani. Inajumuisha itikadi na kanuni zote ambazo mikono yao imezitunga katika kumuasi Mwenyezi Mungu (saw), kama vile demokrasia, usekula, na fahamu za dola za kitaifa na kizalendo.

Sambamba na juhudi za Marekani na washirika wake za kufuatilia na kuandaa watoto wao nchini Afghanistan, raundi ya tatu ya mazungumzo ilianza mnamo Jumapili tarehe 30 Juni 2024 katika mji mkuu wa Qatar, Doha, kati ya maafisa wa Umoja wa Mataifa, wajumbe maalum nchini Afghanistan na wawakilishi wa serikali ya Taliban. Zaidi ya wajumbe ishirini, akiwemo Mwakilishi Maalum wa Marekani kwa Afghanistan, walikutana na ujumbe wa Taliban ukiongozwa na msemaji wake, Zabihullah Mujahid. Kama kawaida, Marekani na mashirika yake ya kikoloni, katika mazungumzo au mipango yoyote, huwasilisha ajenda ya juu juu kwa vyombo vya habari na matumizi ya umma, huku wakificha malengo mbalimbali ya kweli. Nyuma ya lengo lililotangazwa la Marekani la kujadili "haki za wanawake," na dori ya mashirika ya kiraia nchini humo, kuna ajenda ya kuhakikisha dola ya harakati ya Taliban inafuata mipango iliyokubaliwa kati ya Marekani na harakati hiyo, ikiwemo kuigeuza jamii ya kihafidhina ya Afghanistan kuwa ya Kimagharibi, na kuwatumia vibaya wanawake wa Afghanistan katika soko la ajira. Hii ni sawia na kile kibaraka wa Marekani katika Bara Arabu, Salman, na mwanawe mzembe wanachofanya.

Ujinga wa kisiasa haukubaliki tena kutoka kwa vuguvugu, kundi, Mujahid, au mwanasiasa yeyote anayefanya kazi ndani ya Ummah. Hivi ndivyo hali ilivyo sasa kuliko wakati mwingine wowote, kwa vile kila mtu anafahamu ugumu wa njama za kisiasa, na hukmu madhubuti za Shariah, zinazoonya dhidi ya ushirikiano na makafiri, na kukataza kuwaunga mkono. Hakuna yeyote asiyejua ghilba za jamii ya kimataifa dhidi ya Uislamu na Waislamu, kwani haina nia yoyote njema kwetu. Kwa hivyo, hakuna udhuru kwa mtu yeyote!

Sheikh ambaye hivi sasa amefungwa kwenye jela za Mayahudi, mtetezi wa kuasisiwa Khilafah Rashida kwa Njia ya Utume, Sheikh Yusuf Makharza, amesema,
الأعمال الصالحة التي تأتيها في الماضي هي رصيد لك في الآخرة وفي الدنيا، يثني الناس عليك بها ويحبونك لأجلها شريطة أن تبقى في المسار، فإذا كنت أمينا ثم صرت سارقا فإن النكير عليك يكون أعظم من النكير على من قضى عمره سارقا، وإذا كنت مجاهدا ثم صرت نصيرا للعدو تعينه على إخوتك فإياك أن تظن للحظة أن تاريخك أو تاريخ جماعتك يشفع لك، فكل نفس بما كسبت رهينة والتعاون مع العدو يسقط هيبتك ويذهب بكرامتك ويُحل عرضك ويُجرى عليك خلق الله، فالتوبة التوبة قبل فوات الأوان "Matendo mema uliyoyafanya zamani ni mali yako Akhera na duniani. Watu watakusifu na kukupenda kwayo, mradi tu ubaki kwenye njia iliyo sawa. Ikiwa ulikuwa mwaminifu, kisha ukageuka kuwa mwizi, hukumu juu yako itakuwa kubwa zaidi kuliko ile ya mtu ambaye alitumia maisha yake yote kama mwizi. Iwapo ulikuwa Mujahid kisha ukawa mshirika wa maadui, ukawasaidia dhidi ya ndugu zako, ole wako usifikiri hata kidogo kwamba historia yako au ya harakati yako itakushufaiya. Kila nafsi imewekwa rehani kwa iliyo yachuma. Kushirikiana na adui kunaharibu utu wako, kunabatilisha heshima yako, na kukufanya udharauliwe na watu. Kwa hiyo, tubu kabla hujachelewa."

Hivyo basi, viongozi walioghafilika wa harakati ya Taliban lazima warekebishe mwenendo wao. Ni lazima wakubali kile walichokikataa mwanzoni pale Hizb ut Tahrir ilipojitolea kusimamisha Khilafah kwa Njia ya Utume. Ikiwa uongozi wa vuguvugu hautarekebisha njia zake, wanachama waaminifu wa vuguvugu, ambao ni wengi, lazima warekebishe mikengeuko ya viongozi wao. Ni lazima wakabidhi mamlaka kwa wanasiasa waaminifu na wenye uwezo wa Hizb ut Tahrir. Hayo yatawapatia ridhaa ya wakaazi wa ardhini na mbinguni.

Mtume (saw) amesema,

وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَتَأْمُرُنَّ بِالْمَعْرُوفِ وَلَتَنْهَوُنَّ عَنْ الْمُنْكَرِ أَوْ لَيُوشِكَنَّ اللَّهُ أَنْ يَبْعَثَ عَلَيْكُمْ عِقَابًا مِنْهُ ثُمَّ تَدْعُونَهُ فَلَا يُسْتَجَابُ لَكُمْ

**"Naapa kwa Yule ambaye nafsi yangu imo mkononi mwake, lazima muamrishe mema na lazima mukataze maovu, au Mwenyezi Mungu atakuteremshieni adhabu kutoka Kwake; kisha mtamuomba, naye hatakujibuni."** [Tirmidhi]